

**Dondoo za mkutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam
17 Mei 2008**

Mahudhurio

Ally Athuman Jumbe
Ally Saidi Mohamedi
Ally Saidi Mwishehe
Aseli Wilison
Edgar R Paulo
Elaine Baker
Filbert Mbecha
Hamadi Hatibu Bwaja
Husein Hamza Hamisi
Juma Ali Salehe Jongo
Kibwana Mohammad Msiga
Mussa Omari
Paulo Atibu Hatibu
Ramadhani Rajabu Nyengo
Rashidi Saidi Karanji
Sange

Ofisi

Mwenye nyumba wa ofisi yetu alileta barua ofisini wakati wa wiki kusema anataka tuondoke wakati mkataba wetu unamaliza tarehe 1 august 2008. Tulimpigia simu lakini alisema kwamba familia yake wanataka kujenga upya kioski zote kwenye eneo. Hii ilisababisha wasi wasi kubwa kwa wanachama. Jumanne pia anaambiwa kutoka kioski yake ya jirani ya fundi guta.

Wanachama tulikubali kwamba ni nzuri kubaki kwenye eneo sawa kwa sababu imeshajulikana kwamba UWABA ina ofisi Mabibo. Jumanne alisema kwamba kuna jirani moja yupo tayari kuturuhusu kujenga kioski kwenye ardhi yake na tunalipa gharama za ujenzi baadala ya kodi ya miaka kiasi fulani, lakini hii inaweza kuwa na gharama zaidi ya shilingi milioni moja na UWABA haina. Ally Saidi Mohammed alisema atatafuta chumba kinaofaa kwenya mtaa sawa. Tunaweza kuhamisha rafu na bao za tangazo lakini tutakuwa tumepoteza gharama za kupaka rangi.

Mradi wa Usalama Barabarani - Wamba Memorial Fund

Ijumaa Juma aliangalia benki na kipindi cha kwanza cha hela (Tsh 3,575,000) imefika kutoka Wamba Memorial fund. Elaine atawatumia email kuwashukuru.

Husein Hamisi alisema kwamba kuna shule nyingine Kigamboni inaitwa Kidete Secondary School ambapo wanafunzi wanaenda shuleni na baisikeli. Alipendekeza tuandike barua kutambulisha UWABA na kueleza mradi kwa ajili ya shule ili waalimu wakuu wanaweza kuelewa vizuri. Tunaweza kuacha jina la shule wazi ili tutumie barua kwa ajili ya shule mbali mbali. Elaine alikubali kuandika barua hii.

Markus alitembelea HUWATA na walisema wanapenda kuzunguka kutafuta shule lakini wanahitaji hela ya usafiri kwa sababu hawapandi baisikeli. Kwenye badjeti kuna Tsh 50,000 kwa ajili ya gharama za utawala za HUWATA basi tunaweza kuwapa ili watumie kwa ajili ya gharama hizi na gharama zingine za utawala.

Andrew kutoka Ben Bikes alisema ataweza kuja mwezi wa saba. Elaine atashughulikia kwa email.

Tuna mpango wa kwenda Mbondole Secondary School jumamosi ijayo. Wanachama kumi walisema watakuja. Ally Athman anajua njia na Hussein Hamisi atakuja na vifaa vya ufundi wa baisikeli. Tulikubali kutana saa 12 asubuhi jumamosi ijayo.

Traffic police

Elaine, Juma na Markus walienda kutana na Bwana Balele, mkuu wa usalama barabarani siku la jumanne. Alikuwa alisema kwa simu kwamba atakuwepo lakini hakuwepo ofisini hata kama tulisubiri masaa matatu. Basi tuliomba tuonane na mtu mwingine. Tuliongea na mkuu wa stesheni ile.

Tuliuliza kuhusu shida ya magari wanaopaki kwenye service road na alisema kwamba hii hairuhusiwi. Alitupa kipeperushi chenye namba za simu kupiga kutoa repoti ya makosa. Markus alifanya photocopy mbili, lakini Elaine alisahau kuziletea mkutano – ataletea siku nyingine. Hajajibu vizuri maswali kuhusu kama kuna sheria ndogo ndogo na regulations ambazo zina details zaidi kuliko Sheria ya Road Traffic Act, na kama zipo wapi zinapatikana. Tulipomwuliza kuhusu wapi sheria inasema baisikeli zindeshe – kwenye service road au kwenye barabara kubwa alisema inategemea alama za barabara zinasemaje. Tulisema kwamba kwenye barabara nyingi hakuna alama kuonyesha baisikeli zipite wapi.

Wanachama walitoa mifano ya barabara ambapo magari yanapaki njiani na tulizungumza kuhusu shida hii.

Mambo ya hela

Juma alipokea hela ya guta ya Tsh 7,000. Alitumia Tsh 3,500 kununua helmet ndogo kwa ajili ya Mussa Alex. Sasa ana hela ya UWABA ya Tsh 32,500.

Waziri mpya wa Miundombinu

Ally Athman alisema kwamba waziri mpya wa Miundombinu ni Shukuru Kawambwa na naibu yake ni Ezekiel Chibulunje. Waziri wa Miundombinu wa zamani Andrew Chenge aliondolewa kwa sababu alifanya rushwa.

Mambo mengine

Tulimpa Mussa Alex helmet ndogo na tulimhamasisha avae wakati anaendesha baisikeli.

Bwana Wemba wa Chuo cha Usafirishaji alitembelea ofisi yetu wakati wa wiki na alisoma bao za tangazo zetu.

Markus alinunua ramani kubwa za Dar es Salaam kwa ajili ya UWABA.

Elaine aliandaa vitambulisho viwili.

Elaine bado hajatoa nakala za picha za uzinduzi wa ofisi.